# TAMISEMI YA Samia

Maendeleo yanayoonekana

Toleo Na. 10 | www.tamisemi.go.tz | Oktoba 15, 2025






# SAFU YA WACHANGIAJI

Paulo Zahoro -Mwanza
2 Angela Msimbira - Morogoro
3.Elinipa Lupembe -Arusha
4 Salimu Ramadhan - Kagera

# Dibaji

Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amefanya mapinduzi makubwa ya maendeleo na kuboresha maisha ya wananchi.

Wananchi kwenye mikoa yote wameendelea kufurahia maboresho makubwa ya huduma za jamii zinazogusa maisha ya kila siku.Maboresho hayo yamegusa maeneo ya huduma za usafiri na usafirishaji, kwa sasa Tanzania inafikika popote tena kwa urahisi zaidi, huduma za maji, ongezeko la shule, vituo vya afya na zahanati ni jambo ambalo limefupisha umbali wa wananchi kwenda umbali mrefu kupata huduma hizo.

Ni kwa msingi huu, ninayo furaha kubwa ya kukuletea jarida hili la Wizara ya TAMISEMI, liitwalo "TAMISEMI YA SAMIA: Mabadiliko yanayoonekana" ambalo jina lake linaakisi na kuonyesha wazi uongozi wake, mabadiliko yaliyofanyika na kwamba maendeleo hayo ni dhahiri nayanagusa wananchi wote.

Toleo hili la kumi linaangazia mafanikio makubwa ya shughuli mbalimbali yaliyopatikana kwenye maeneo ya elimu, afya na miundombinu kwenye mikoa ya Mwanza, Arusha Kagera na Morogoro.

Ninawatakia usomaji mwema
Mungu ibariki Afrika!
Mungu ibariki Tanzania!

John J. Mapepele
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano - TAMISEMI

# OFISI YA RAIS,
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# (OR - TAMISEMI)

ortamisemi




# RAIS SAMIA AWALETEA WANANCHI MELI YA KISASA KUIMARISHA USAFIRI NA USAFIRISHAJI ZIWA VICTORIA

Na Paulo Zahoro - Mwanza

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhe. Said Mtanda ameshuhudia jaribio la mwisho la safari ndefu kwa Meli ya MV New Mwanza kwenye bandari ya Mwanza Kusini kuelekea kwenye Bandari ya Bukoba (Neutical Miles 100) baada ya kuletwa na Serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza na wananchi waliojitokeza kushuhudia hafla hiyo ya kihistoria Mhe. Mtanda amesema kukamilika kwa meli hiyo ni ishara ya juhudi za serikali katika kuimarisha sekta ya usafiri wa njia ya maji na usafirishaji wa abiria na mizigo katika ukanda wa ziwa Victoria.

Aidha, amesema wananchi wa Mwanza na ukanda wa ziwa Victoria kwa ujumla wamepata usafiri wa uhakika na kuondokana na adha ya ajali zilizotokana na matumizi ya usafiri duni wa mitumbwi na kwamba nauli zitakua nafuu sana kwa safari za ndani na nje ya nchi kama ilivyo dhamira Mhe. Rais Samia ya kuboresha sekta ya usafiri kwa njia ya maji.

Ameongeza kuwa katika kuhakikisha ukanda huo unakua salama katika usafiri, usafirishaji na hata uvuvi serikali kwa kushirikiana na nchi wanachama wa Jumuiya Afrika Mashariki wanajenga kituo maalum cha uokozi katika eneo la Malaika Beach kwa gharama ya zaidi ya Bilioni 5.

Mhe. Mtanda amebainisha kuwa meli hiyo yenye uzito wa tani elfu nne (4000) na ghorofa nne, ina uwezo wa kubeba abiria 1200, Magari 20 madogo, Malori 3 imejengwa na watanzania zaidi ya 200 waliooshirikiana na timu ya wataalamu 16 tu wa mkandarasi kutokea nchini Korea Kusini.

Sambamba na hayo ameongeza kuwa pamoja na changamoto kama za kupanda kwa gharama za vifaa kama vyuma na wataalamu kushindwa kufika kwa wakati hatimaye meli hiyo ya kisasa yenye urefu wa mita 92.6 yenye spidi kubwa leo hii imekamilika na itafika Bandari ya Bukoba kwa saa 6 pekee.






# BILIONI 3.4 ZA RAIS SAMIA KUTATAU CHANGAMOTO YA HUDUMA ZA AFYA MISSENYI

Na Salimu Ramadhani - MISSENYI DC

Katika kuimarisha huduma za Afya katika Wilaya ya Missenyi, Serikali ya awamu ya sita imetoa jumla ya shilingi bilioni 3.4 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali Mpya ya Wilaya ya Missenyi ili kuimarisha huduma za afya Wilayani humo.

Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya umefikia asilimia 98 huku ukijujmuisha majengo 12 ambayo ni Jengo la Utawala, Upasuaji, Dawa,Kufulia,Maabara, Mionzi, Upasuaji, Jengo la Wagonjwa wa nje, Wagonjwa wa Dharura, Wodi ya Wanawake, Wanaume na Wodi ya Watoto.

Aidha, mpaka sasa Hospitali hiyo imeshapokea vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi milioni 800, watumishi 39 na huduma za awali zimesha anza kutolewa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi Bw. John Paul Wanga akizungumza katika kikao kazi kilichoikutanisha Timu ya Menejimenti ya Halmashauri na kamati ya usimamizi wa huduma za Afya ngazi ya Wilaya (CHMT) alimpongeza Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutupatia fedha hizo kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa vifaa tiba ili kuboresha huduma za afya katika Wilaya ya Missenyi.

“Naishukuru sana Serikali ya awamu ya sita kwa kutatua changamoto ya kufuata huduma kwa umbali wa wastani wa kilomita 80 hapo awali hadi kufikia wastani wa kilomita 40 kwa sasa na hali hii itapunguza vifo vya mama na mtoto kutokana na kupatikana kwa huduma kubwa zaidi ambazo tulizikosa kwenye vituo vya afya.” Alisema Bw. Wanga

Aidha, Bw. Wanga aliwataka wataalam kuhakikisha wanasimamia Pamoja na kuweka mipango mizuri ili kuhakikisha huduma lengwa inamfikia mwananchi kama serikali ilivyokusudia.
Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Missenyi Dkt. Daniel Chochole alisema Hospitali yetu inatarajia kuhudumia wakazi wapatao 245,394 huku wakinufaika na uwepo wa huduma za upasuaji, kupungua kwa gharama za matibabu ukilinganisha na huduma walizokuwa wanapata katika Hospitali binafsi pamoja na kupunguza vifo vya mama na mtoto vitokanavyo na uzazi.

Ikumbukwe kwamba hapo awali wananchi wa Wilaya ya Missenyi walikua wanapa Huduma za Hospitali ya Wilaya kutoka Hospitali Binafsi ya Mugana iliyopo takribani kilomita 80 kutoka makao makuu ya Wilaya.



# WALIMU WA ARUSHA WAMPA MAUA YAKE RAIS SAMIA KWA KUBORESHA ELIMU

Na Elinipa Lupembe - Arusha

Walimu Mkoa wa Arusha wamekiri kuwa, Serikali ya awamu ya sita chini ya Mhe.Dkt.Samia Suluhu Hassan, imefanya mapinduzi makubwa katika sekta ya elimu, tofauti ni huko nyuma, jambo ambalo licha ya kupandisha taaluma na kuongeza idadi ya wanafunzi, limeamsha ari ya walimu na wanafunzi katika tendo la kufundisha na kujifunza.

Haya yamewekwa wazi na walimu wa mkoa huo, wakati wa Kongamano la Wadau wa Elimu kuelekea juma la elimu Mkoa wa Arusha, lililofanyika kwenye ukumbi wa mikutano Ofisi ya Mkuu wa Mkoa huo, hivi karibuni wamethibitisha kuwa, katika awamu ya sita, imejengwa shule mpya za msingi 14 na sekondari 27, uwepo wa vifaa vya kisasa vya kujifunzia na kufundisha, ujenzi wa nyumba za walimu, upandishaji wa vyeo kwa walimu pamoja na fedha za uendeshaeji elimu bila malipo zilizopelekea ongezeko la idadi ya wanafunzi shuleni.

Mwenyekiti wa Umoja wa shule za Msingi TAPSHA Mkoa wa Arusha, Mwalimu Amani Palangyo amesema kuwa, uwepo wa miundombinu bora, rafiki na ya kisasa shuleni unawapa moyo walimu kufundisha kwa bidii pamoja na kujenga uhusiano mzuri baina ya mwalimu na wanafunzi unaorahisisha tendo la kufundisha na kujifunza.

"Mimi kama mwalimu ninayefundisha darasani pamoja na walimu wenzangu tunayo makubwa ya kushuhudia yaliyofanywa na serikali ya awamu ya sita, kwa sasa tunafundisha kwenye madarasa mazuri, madarasa makini yenye vifaa vya kisasa vya kielekroniki vya kufundishia, walimu wanaishi shuleni kwenye nyumba nzuri za kisasa, hakika walimu hatujaachwa nyuma".Amesisitiza Mwalimu Palangyo.

Naye Mwenyekiti wa Umoja wa Walimu wa Shule za Sekondari (TAHOSA) Mkoa wa Arusha na Mkuu wa shule ya Sekondari Kiranyi Mwalimu Omari Nyigu amesema kuwa, kwa kipindi cha miaka 4, idara ya elimu sekondari imepokea shilingi bilioni 64.1 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya shule, miundombinu ambayo imeongeza ari ya wanafunzi kujifunza na walimu kufundisha.

Kaimu Afisa Elimu Mkoa wa Arusha Mwalimu Tumsifu Mushi, ameweka wazi kuwa katika kipindi cha miaka 4 ya serikali ya awamu ya sita, sekta ya elimu imepokea jumla ya shilingi bilioni 267 kwa ajli ya sekta ya elimu, shilingi bilioni 107 zikitumika katika ujenzi na ukarabati wa miundombinu huku bilioni 168.2 fedha kwa ajili ya utekelezaji wa elimu bila malipo.

Amefafanua kuwa, kwa miaka minne kumekuwa na uboreshaji mkubwa wa miundombinu ya shule, ikiwa nipamoja na kujenga shule mpya 27 za sekondari, shule mpya 14 za msingi, vyumba vipya vya madarasa 843, mabweni 60, maabara 78, majengo ya Maktaba 26, majengo ya TEHAMA 26, majengo 26 ya nyumba 27 za walimu pamoja na matundu ya vyoo 940.



# SERIKALI YAWASHAURI WALIMU NA JAMII KUIMARISHA USALAMA WA WATOTO SHULENI

Na Angela Msimbira- Morogoro

Serikali imeendelea kusisitiza umuhimu wa kutekeleza Mpango wa Shule Salama nchini, ikitoa wito kwa walimu wakuu, wenyeviti wa kamati za shule na jamii kuhakikisha usalama wa watoto unazingatiwa kama kipaumbele cha kwanza katika mazingira ya shule.

Akizungumza wakati wa mafunzo kuhusu mpango huo, Mkufunzi Mkuu wa Chuo cha Ualimu Mpwapwa, Juma Kizija, amesisitiza kuwa usalama wa mtoto shuleni ni wajibu wa pamoja unaohitaji mipango madhubuti na ushirikiano wa karibu kati ya wadau wote wa elimu.

Kizija amewashauri walimu wakuu kuandaa mikakati ya mapema ya kuboresha miundombinu, ikiwemo kuhakikisha madarasa, vyoo, njia za kupitisha wanafunzi na maeneo ya michezo yanakuwa salama, rafiki na yenye kuzingatia utu wa mtoto.

Aidha, amesisitiza kuwa kamati za shule zinapaswa kushirikiana kikamilifu na wazazi na jamii ili kubaini mapema changamoto za kiusalama na kuzitafutia ufumbuzi wa pamoja. “Shule siyo jengo pekee, bali ni kituo cha malezi, ulinzi na ujenzi wa tabia. Kila hatua ya maendeleo lazima izingatie haki na usalama wa mtoto,” amesema

Walimu wakuu pia wamekumbushwa kuwa na mifumo thabiti ya kuripoti matukio ya ukatili, manyanyaso au viashiria vyovyote vya hatari dhidi ya wanafunzi, pamoja na kuwapa watoto elimu ya tahadhari juu ya usalama wao wakiwa shuleni na wanaporudi majumbani.

Kizija ametoa wito wa kuachana na dhana ya kuiachia shule jukumu la malezi, akisema malezi bora hufanikiwa pale ambapo wazazi wanashiriki kikamilifu katika mikutano, maamuzi na shughuli za shule.

Amesisitiza kuwa mafanikio ya elimu hayatafikiwa iwapo watoto hawapo katika mazingira salama. Kujenga kizazi chenye nidhamu, maarifa na matumaini ya baadaye kunahitaji shule zinazolinda utu, usalama na haki za mtoto.

Kupitia ushirikiano wa walimu, wazazi na viongozi wa shule, Mpango wa Shule Salama unaweza kufanikisha mabadiliko chanya na kuchochea mustakabali mwema wa elimu nchini.



# SERIKALI YABORESHA HUDUMA ZA MAJI MWANZA

Na Paulo Zahoro -Mwanza

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe. Said Mtanda amesema Serikali inaendelea kuboresha na kuimarisha huduma ya maji kwa wanachi wa mkoa huo kwa kurabati vyanzo vya maji vya Butimba na Capripoint ambavyo ni vyanzo vikubwa vyakusambaza maji katika maeneo yote ya mkoa huo.

Mhe. Mtanda amesema hayo wakati akikagua chanzo cha maji Butimba ambacho kinazalisha maji safi lita Millioni 48 kwa siku na kusambaza huduma hiyo katika maeneo ya Nyegezi, Buhongwa, Mkolani na Mkuyuni na kujihakikishia kuwa huduma hiyo inapatikana kwa wananchi wa maeneo yote.

Aidha, Mhe. Mtanda amesema serikali inaendelea na mchakato wa kupanua na kuboresha mradi wa maji wa Capripoint uliofikia asilimia 35 mpaka sasa ambao ulikua ukizalisha maji Lita Millioni 90 kwa siku na baada ya marekebisho utazalisha maji Lita Millioni 138 kwa siku.

Ameongeza kuwa mafundi na wataalamu wanaendelea kufanya kazi mchana na usiku kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji kama kawaida kwa kuendelea kutatua changamoto na hitilafu ambazo zinajitokeza katika mifumo na mitambo ya maji.

Sambamba na hayo Mhe. Mkuu wa Mkoa akiwa ameambatana na Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA walihitimisha ziara kwa kuwatembelea baadhi ya maeneo ya wananchi na kuendelea kujiridhisha kuwa huduma inapatikana kwa wananchi kama ilivyokawaida.

www.tamisemi.go.tz